

GRADE 3 -YEAR 2022

EXAMINATION: KISWAHILI ACTIVITIES

NAME: _____

SEHEMU 1: KUSIKILIZA NA KUONGEA

Mwalimu amuulize mwanafunzi maswali yafuatayo.

1. Habari yako?
(Mwanafunzi ajibu)
2. Taja tunda unalolipenda.
(Mwanafunzi ajibu)
3. Tunda hilo linapatikana wapi?
(Mwanafunzi ajibu)
4. Kabla ya kula tunda unafaa ufanye nini?
(Mwanafunzi ajibu)
5. Tunda hilo huwa tamu likiwa bivu au bichi?
(Mwanafunzi ajibu)

SEHEMU 2: KUSIMA KWA SAUTI

Soma kifungu hiki kwa sauti

Niliamka asubuhi na mapema. Kulikuwa na utulivu kwa sababu watu wengi hawakuwa wameamka. Hata wazazi wangu bado walikuwa wakilala. Nilienda bafuni nikaoga. Kisha nikaenda jikoni kutayarisha staftahi. Sikutaka nichelewe kufika shuleni. Baada ya kupata staftahi, nilipiga meno mswaki kisha nikavaa sare za shule. Nilitoka mbio hadi shuleni. Siku hiyo ilikuwa siku ya kuzuru mbuga ya wanyama.

SEHEMU 3: UFAHAMU

Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.

Hapo zamani za kale, kuku na mwewe. Walikuwa marafiki wa chanda na pete. Walikuwa wakiishi pamoja. Kila asubuhi walienda kulima katika shamba lao. Kuku alikuwa na vifaranga watano naye mwewe alikuwa na makinda wawili. Siku moja kuku alimkanyaga kinda mmoja hadi akaaga dunia. Ingawa ilikuwa ajali, mwewe aliapa kulipiza kisasi. Kuku aliamua kutoroka hadi kwa binadamu. Tangu siku hiyo, mwewe huwashika vifaranga wa kuku kulipiza kisasi.

1. Kila asubuhi kuku na mwewe walienda wapi?
2. Kuku alikuwa na vifaranga wangapi?
3. Mwewe alikuwa na makinda wangapi?
4. Nani alimkanyaga kindi?
5. Kuku alitoroka hadi wapi?

SEHEMU 4: SARUFI

Kanusha sentensi.

1. Enda nyumbani.
2. Mtoto anakula ndizi.
3. Baba analima shambani
4. Kaka amepika chakula
5. Soma kitabu hiki.

Andika kinyume.


6. Shuka
7. Rudi
8. Ketu
9. Funika
10. Jenga

Andika tarakimu kwa maneno.

11. 86
12. 92
13. 126
14. 74
15. 225

Andika majina ya maumbo haya.


16.




17.



18.



19.



20.

